

**HOTUBA YA JAJI MKUU MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA  
SIKU YA SHERIA, DAR ES SALAAM,  
TAREHE 06 FEBRUARI, 2019**

***Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

***Mhe. Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

***Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,***

***Mhe. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar,***

***Mhe. Jaji Kiongozi,***

***Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,***

***Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria,***

***Mhe. Prof. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,***

***Mhe. Eng. John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi***

***Wahe. Makamishna wa Tume ya Utumishi Mahakama***

***Wahe. Majaji Wakuu wastaafu***

***Wahe. Majaji wa Rufaa, Majaji Viongozi Wastaafu***

***Wahe. Majaji Wastaafu,***

***Wahe. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria***

***Wahe. Mabalози na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,***  
***Wahe. Viongozi wa Dini mbalimbali na vyama vya siasa,***  
***Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,***  
***Mhe. Mtendaji Mkuu na Msajili Mkuu Mahakama ya Tanzania,***  
***Mkurugenzi wa Mashtaka,***  
***Wakili Mkuu wa Serikali,***  
***Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama,***  
***Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,***  
***Wasajili,***  
***Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,***  
***Mhe. Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar,***  
***Mahakimu wa ngazi mbalimbali,***  
***Viongozi Wandamizi wa Serikali,***  
***Mawakili wa Serikali na Wa Kujitegemea,***  
***Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika,***  
***Viongozi wa vyama vya Siasa,***  
***Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.***

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Rais**, hapana budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya, nguvu na siha na kuweza leo kukutana tena katika Siku hii ya Sheria nchini kwa mwaka 2019.

Kwa niaba yangu binafsi na Mahakama kwa ujumla, ninayo heshima kubwa kukushukuru kwa kukubali mwaliko wangu kwa mwaka wa nne mfululizo bila kujali ratiba nyingi na ngumu ulizo nazo. Hii ni ishara kubwa kwamba unatekeleza kwa vitendo, yale uliyosema katika Hotuba yako ya tarehe 20 Novemba, 2015 ulipofungua rasmi, Bunge la Jamhuri ya Muungano. Baadhi ya mambo muhimu kwetu uliyoyatamka – Serikali ya Awamu ya Tano itaheshimu na kukendeleza utamaduni mzuri uliojengeka nchini wa kuheshimu mihimili ya dola; kwamba Serikali yako, italipa uzito mkubwa suala la uboreshaji wa Mahakama kwa kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi; kuongeza kasi ya utoaji haki.

## **2.0 KAULI MBIU MWAKA 2019**

**Mheshimiwa Rais**, Kila nchi inayoazimia kuwa na uchumi unaokuwa kwa kasi, ni lazima migogoro inayowasilishwa Mahakamani ikamilike kwa haraka, na wananchi watumie muda wao mwingi zaidi na rasilimali zao, kuzalisha mali na kutoa huduma badala ya kupoteza muda wao wa wakitafuta utatuzi Mahakamani. Kumekuwa na dhana kuwa mashauri ya jinai na madai yanapochelewa kukamilika mahakamani, basi ni mahakama tu ndiyo inayochelewesha utoaji haki. Kauli mbiu ya mwaka huu ya ***“Utoaji haki kwa wakati, Wajibu wa Mahakama na Wadau”***

inajenga hoja kwamba, wadau wote muhimu katika mnyororo wa utoaji haki wana mchango mkubwa sana katika kuharakisha utoaji haki na kazi ya Mahakama ya utoaji haki haitafanikiwa kwa juhudi za Mahakama peke yake. Kazi ya utoaji haki inayohusisha wadau mbalimbali. Wadau hao, wakitimiza wajibu wao kwa wakati, wanaiwezesha mahakama kumaliza mashauri na mwanachi kupata haki yake kwa wakati. Wadau hao ni **Wizara ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (AGC & SG), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka/DPP, Polisi, Mkemia Mkuu, Magereza, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba (W), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Tume ya Kurekebisha Sheria (LRC), Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Bunge, Kamishna wa Kazi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, wengine wengi.**

Serikali yako Mheshimiwa Rais; na Mhimili wa Bunge unaongozwa na Mheshimiwa Spika, ni wadau muhimu na wezeshi kwa Mahakama na utoaji haki.

**Mheshimiwa Rais**, Benki ya Dunia imeendelea kuwa mdau muhimu katika utoaji haki hapa Tanzania. Huu ni mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mahakama na Programu ya Maboresho inayofadhiliwa na Benki ya Dunia inayosukumwa na dhana ya kupeleka HUDUMA ZA HAKI kuwa karibu na wananchi

(kwa Kiingereza — Citizen-Centric Justice). Napenda kukutambulisha kwako Mama Bella Bird, Mkurugenzi Mkazi Benki ya Dunia na timu yake ya hapa nchini. Napenda pia kuwatambua wajumbe kutoka Makao Makuu ya Benki ya Dunia, Washington ambao wamejumuika na sisi leo hii; ambao ni— Deborah Isser; Denis Biseko, Waleed Malik, Bilal Siddiq, Clara Maghani na wengine wote.

**Mheshimiwa Rais,** nimewahi kusema huko nyuma kuwa huduma bora za haki pia zinategemea ushiriki mkubwa na wa karibu, wa wananchi. Utoaji haki kwa wakati utawezekana pale ambapo wananchi wenye mashauri mahakamani, wanafuata taratibu za kimahakama za uendeshaji mashauri, wanahudhuria Mahakamani kadri wanavyoitwa, wanawasilisha ushahidi wao kwa wakati, na wasiporidhika na uamuzi wa ngazi moja ya mahakama, wanakata rufaa ndani ya muda uliowekwa kisheria. Hii yote itawezesha Mahakama kuwahudumia kwa wakati, na kwa ubora zaidi. Napenda kuchukua fursa hii na kutoa wito kwa kila mwananchi, tujisomee sheria ili tuwe na uelewa angalau kidogo wa sheria(General legal literacy). Tusiwaachie mawakili na wanasheria peke yao jukumu la kufahamu taratibu za sheria. Tunapokuwa na jambo linalohusu sharia, mathalan ya mirathi, hatua ya mwanzo kabisa ni mwananchi asome vifungu vya sheria husika yeye mwenyewe na apate uelewa yeye mwenyewe kabla ya kupata tafsiri kutoka kwa wakili au mwanasheria. Kabla ya kufungua shauri

Mahakamani, mwananchi ahakikishe kuwa anafahamu hatua zote kesi yake itapitia katika ngazi ya Mahakama zote hadi Mahakama ya Rufani. Hauhitaji elimu ya Sheria kujua hatua muhimu ambazo kesi zako zitapitia.

Hapa, **Mheshimiwa Rais**, nina ombi maalum kwa **Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali**: aweke *Sheria zote za Tanzania Mitandaoni, kama sehemu ya Serikali Mtandao*. Hatua hii itamuwezesha mwananchi aweze kusoma sheria zinazogusa maslahi yake kwa wakati wake, na ataweza kujua angalau baadhi ya hatua na taratibu muhimu zinazohusu kesi yake iliyo Mahakamani.

### **3.0 MATUMIZI YA TEHAMA**

**Mheshimiwa Rais**, hakuna anayeweza kubisha kuwa matumizi ya TEHAMA yana msaada mkubwa katika kuharakisha utoaji haki kwa wakati, na pia yanasogeza huduma za Mahakama karibu zaidi na wananchi. TEHAMA italeta mapinduzi haya ya utoaji haki pale tu Mahakama itashirikiana kwa karibu na wadau na wananchi.

Katika matumizi ya TEHAMA kwenye utoaji haki, Mahakama imetoka kwenye nadharia na imeingia katika vitendo kwa kutenda. Mfumo ya kielekitroniki wa kusajili na kuratibu mashauri - **JSDS II**) tayari unafanyakazi. Mfumo huu unawezesha kufanyika kwa urahisi kwa mambo mbalimbali ya usimamizi wa Mashauri kama; kufungua shauri kielekitroniki, na hata kuitwa shaurini/kupata

taarifa za shauri kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu – (*sms notification*). Kupitia Mfumo huu wa ki-elektroniki, benki ya kuhifadhi hukumu – (*Judgement database*) inafanya kazi. Matumizi ya TEHAMA kwa vitendo yanaonekana pia kwenye MFUMO WA KUSAJILI NA KURATIBU MAWAKILI (TAMS) na pia kutengenezwa kwa MFUMO WA KI-ELEKTRONIKI WA UTAMBUZI WA MAHITAJI YA MAHAKAMA (*COURT MAPPING*) uliyotayarishwa chini ya ushauri wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU). Majaji wa Mahakama ya Rufani na Majaji wafawidhi kutoka kanda zote za Mahakama Kuu na Divisheni pamoja na watumishi wa kada nyingine zote wamepata Semina Elekezi kwenye Maboresho na mabadiliko haya muhimu ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa kutumia MFUMO WA UKUSANYAJI WA TAKWIMU ZA MASHAURI/KESI KWA MIFUMO YA KIELEKITRONIKI (**JSDS II**), haitakuwa lazima mtu kusafiri umbali kufungua shauri kwenye Mahakama Kuu za Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma na Mahakama ya Hakimku Mkazi Kisutu. Hata hivyo, baada ya muda mfupi Mahakama zetu zote zitafikiwa.

**Mheshimiwa Rais,** mfumo huu wa **JSDS II** unatuwezesha kujua kila Mahakama imefanya nini kila siku na kila Jaji au Hakimku amefanya nini. Tunajivunia mfumo huu kwa sababu kuu mbili. **Moja,** unasaidia sana usimamizi wa Mashauri. **Pili,** umejengwa na

vijana wetu - watumishi wa Mahakama, hivyo mfumo huu unamilikiwa na Mahakama asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Rais**, tunatambua jitihada za Serikali za kuleta nidhamu kwa watumishi, kuondoa watumishi hewa na kusimamia utendaji kazi wa watumishi. Mahakama iliona iende mbali zaidi kwa matumizi ya teknolojia. Kupitia mfumo wetu wa ki-elektroniki wa utambuzi wa mahitaji ya Mahakama **Court Mapping**, nikiwa hapa Dar es Salaam, naweza kupata taarifa zote zinazohusu mahakama yoyote kuhusiana na watumishi, hali ya majengo, umbali kutoka Makao Makuu ya Mkoa na kadhalika. Mfumo huu unatuwezesha si kujua tu Mahakama zetu; zaidi, unatuwezesha kupata taarifa sahihi na kufanya maamuzi kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais**, makusanyo yote ya Mahakama (*Revenue*) na malipo ya ada zote za Mahakama yameanza kufanyika kwa njia ya ki-elektroniki kupitia mfumo wa malipo wa Serikali maarufu kama *Government Electronic Payment Gateway (GePG)* kwa kuanzia na mkoa wa Dar es salaam. Mfumo huu, umeunganishwa na mfumo wetu wa usimamizi wa mashauri (*case management system*). Hakuna kesi yoyote, kwa mfano inaweza kusajiliwa bila kulipia ada.



**Mheshimiwa Rais**, tangu tumejiunga na utaratibu huu wa malipo maduhuli yameongezeka toka shilingi **1,629,809,490.41** kwa kipindi cha mwezi Julai – Desemba, 2017 (kupitia Benki) hadi kufikia shilingi **2,164,197,696.90** kwa kipindi cha mwezi Julai – Desemba, 2018 (kwa mfumo wa **GePG**).Muda mfupi ujao mfumo huu utafikia mahakama zote nchini.

**Mheshimiwa Rais**, mifumo mingine inayofanya kazi kwa sasa ni; kuanza kusikiliza MASHAURI KWA NJIA YA KIELEKITRONIKI (*video conferencing*) ambapo shauri linaweza kusikilizwa mtuhumiwa akiwa mahabusu/gerezani (Keko); pamoja na kusikiliza mashahidi wakiwa nje ya nchi. Kwa mfano tarehe 05/12/2018 Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara ilimsikiliza shahidi akiwa nchini Ufaransa kupitia *video conferencing* kupitia kituo cha HABARI NA MAFUNZO Kisutu na hivyo kuokoa gharama za kumleta shahidi huyo nchini.

**Mheshimiwa Rais**, mahakama inaendelea kufanya maboresho katika tovuti, mfumo wa kusajili na kuratibu madalali ambapo mifumo yote hii itatufikisha kwenye mpango mkubwa wa kuwa na mahakama mtandao (*e-judiciary*) na hatimaye haki mtandao (*e-justice*) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

#### **4.0 Maendeleo ya watumishi**

**Mheshimiwa Rais**, kutokana na shughuli za mahakama kusambaa karibu kila kona nchini, mahitaji halisi ya watumishi ni makubwa mno. Utafiti unaonesha kwamba, ili mahakama zote nchini zifanye kazi kwa ufanisi kwa upande wa rasilimali watu, watumishi **24,643** wanahitajika. Hata hivyo watumishi waliopo ni **6,096** tu kwa hiyo kuna upungufu wa watumishi **18,556**.

**Mheshimiwa Rais**, pamoja na upungufu uliopo, idadi ya watumishi wa Mahakama imeendelea kupungua siku hadi siku kutokana na sababu mbalimbali hivyo kuendelea kuongeza changamoto ya upungufu wa watumishi. Takwimu za mwezi Januari – Desemba, 2018, zinaonesha kwamba jumla ya watumishi **248** wameondoka kazini kati yao **200** kwa kustaafu na **35** kwa kufariki. Aidha watumishi wengine **194** waliondolewa kazini kwa kuwa na vyeti vyenye kasoro.

**Mheshimiwa Rais**, katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa watumishi, hadi mwezi Desemba, 2018 watumishi **420** walijiririwa. Vilevile tumeomba kibali cha kuajiri watumishi **168** kwa ajili ya Mahakama mpya zinazoanzishwa na wakati huo huo tuna nafasi wazi za ajira mbadala **420** ambazo maombi yake yaliwasilishwa kwenye mamlaka husika. Bado tunasubiri majibu.

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama imeendelea na jitihada za kusimamia nidhamu ya watumishi wake katika maeneo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2018 watumishi **81** walikuwa wanakabiliwa na mashauri ambapo kati yao mashauri **40** ni ya jinai na yanayoendelea katika Mahakama mbalimbali.

### **Rushwa Sehemu ya Kazi:**

**Mheshimiwa Rais,** katika kupambana na rushwa sehemu za kazi, mahakama imehakikisha inaandaa Mpango wa Kupambana na Rushwa ikiwa ni utekelezaji wa kufanyia kazi maelekezo yaliyomo kwenye Mpango wa Taifa wa Kupambana na Rushwa Nchini **(NASCAP III)**. Pamoja na mpango huo kuendelea kuandaliwa, tayari watumishi Mahakimu **8** wenye mashauri ya jinai ya rushwa kesi zao zipo Mahakamani. Majaji Wafawidhi tayari wamekumbushwa kuwa pamoja na kusimamia utoaji HAKI kwa wakati sehemu wanazosisimamia, wanayo jukumu la kusimamia maadili, kuziba mianya ya rushwa na kuchukua hatua za awali kwa mujibu wa sheria.

### **Mafunzo Endelevu:**

**Mheshimiwa Rais,** kwa kuzingatia kwamba kazi za Mahakama zinahitaji ujuzi endelevu, imekuwa kawaida sasa kwa Mipango ya Mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi huandaliwa na Chuo chetu cha Mahakama cha Lushoto (IJA). Katika kipindi cha mwaka

2018 watumishi **1,030** na wadau **122** wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi.

**Mheshimiwa Rais**, watumishi **133** wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na maarifa. Idadi hiyo inajumuisha watumishi **64** wanaogharamiwa na mwajiri katika Shule ya Sheria kwa Vitendo (**Law School**) na watumishi wengine **69** wanaojiendeleza kwa gharama zao wenyewe.

Chini ya mradi wa Maboresho unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Mahakama iko mbioni kutayarisha mafunzo maalum kwa Mahakimu wakazi wapatao 503 kutoka Mahakama za Mwanzo, za Wilaya na za Hakim Mkazi. Mafunzo haya maalum yatahusu maeneo ya uandishi wa hukumu (*judgment-writing skills*), utoaji wa adhabu (*sentencing*) na ukazaji wa hukumu.

### **Stahili za Wafanya Kazi:**

**Mheshimiwa Rais**, mahakama imeendelea kuhakikisha kwamba maslahi na haki za watumishi zinapatikana haraka kwa mujibu wa sheria, miongozo na taratibu mbalimbali za utumishi wa umma. Hadi mwezi Desemba, 2018 watumishi **1,211** wamepandishwa vyeo kati yao wapo Mahakimu **540**. Aidha, watumishi **962** kati yao wapo Mahakimu **35** wanasubiri kibali cha Katibu Mkuu (UTUMISHI) ili

wapandishwe vyeo na watumishi wengine **1,006** wametengewa nafasi kwenye mpango wa mwaka 2018/19. Hatua za kuwabadilisha kada watumishi **162** waliojipatia sifa tayari zimechukuliwa kwa utaratibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama.

### **Kuongezeka kwa Idadi ya Majaji:**

**Mheshimiwa Rais**, nitumie fursa hii kukushukuru tena kwa UTEUZI uliufanya mwaka **2018**, wa Majaji wawili **(2)** wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi, na Majaji **12** wa Mahakama Kuu. Aidha kwa mwaka huu wa 2019, tunakushukuru sana kwa NGUVU MPYA uliotujaza kwa uteuzi wa Majaji **6** wengine wa Mahakama ya Rufani na Majaji wengine **15** wa Mahakama Kuu ambao uliwaapisha tarehe 29/01/2019. Sasa, idadi hiyo imeifanya Mahakama Kuu kuwa na jumla Majaji sabini na watatu (73). Idadi ya Majaji wa Rufani sasa imefikia ishirini **(21)** na ni ongezeko la kihistoria kutoka Majaji wa Mahakama ya Rufani kumi na Tano **(15)** idadi iliyokuwepo kwa muda mrefu. Ninaomba tena, idadi hii iongezeke zaidi ya **21**, bila kushuka tena na kurudi kwenye **15**.

## **Maslahi ya Wafanya Kazi:**

**Mheshimiwa Rais,** ulipokuja kuungana nasi kama mgeni rasmi kwenye kilele cha siku ya sheria mwezi Februari, 2018, ulisikia kilio cha watumishi wa ngazi mbalimbali za Mahakama kuhusiana na maslahi mbalimbali ya kikazi na hili ni kutokana na hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya kimahakama ambayo hutofautiana sana na Taasisi nyingi za Umma. Sihitaji kueleza hapa zaidi ya ulichoahidi wakati ukifungua Bunge jipya tarehe 20/11/2015—kwamba utalipa uzito swala la uboreshaji wa maslahi ya watumishi wa Mahakama zetu. Najua unafahamu sana maana kila mara umekuwa ukiniambia kuwa unafahamu hali halisi ya maslahi ya watumishi wa Mahakama.

**Mheshimiwa Rais,** Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa mujibu wa Ibara ya **113** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria Na. 4 (2011) kifungu cha 31(1) na (2) na 32 cha Sheria hiyo, Tume ya Utumishi wa Mahakama ina wajibu wa kukushauri Mhe. Rais, juu ya maslahi, na mishahara ya watumishi wa Mahakama ya Tanzania.

**Mheshimiwa Rais,** nachukua fursa kukukumbusha juu ya mapendekezo yetu kwako kuhusu maslahi na mishahara ya watumishi wa Mahakama. Ushauri wetu kwako ulizingatia hali halisi ya uchumi wa nchi na kufuata mzunguko wa Bajeti ya

Serikali ya mwaka wa fedha 2018/19. Ni matumaini yetu kwamba maombi yetu hayo madogo kwako yatapata Baraka zako tele na watumishi wa mahakama watachapa kazi kwa ari zaidi na uadilifu zaidi.

## **5.0 Usikilizaji wa Mashauri**

**Mheshimiwa Rais,** wajibu wetu wa Kikatiba sisi Mahakama ya Tanzania, ni kutoa haki. Tuna imani kwamba katika kutoa haki tunaimarisha uchumi. Kupitia utoaji haki, tunaimarisha amani, utulivu, utawala wa sheria na upatikanaji wa haki unatoa nafasi kwa wananchi kufanya kazi za kiuchumi ili kujiletea maendeleo binafsi na kuleta maelendeleo ya nchi. Pia, Mahakama inayotoa haki kwa wakati hujenga imani kwa wawekezaji wa kutoka ndani na nje ya Tanzania. Wawekezaji wataavutiwa kuwekeza fedha zao, iwapo kutakuwa na misingi imara ya utoaji haki iliyo bora kwa wakati, na kwa kuzingatia maadili.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa kuzingatia elekezo la kikatiba linaloilazimu Mahakama kuzingatia takwa la kutochelewesha haki bila sababu za msingi, Mahakama imejiwekea sera ya kuhakikisha kuwa mashauri yanapofunguliwa Mahakamani yanakuwa na muda maalum wa kukamilika katika ngazi husika ya Mahakama. Kwa mfano, Mahakama za Mwanzo ziliwekewa malengo ya kumaliza mashauri ndani ya **miezi sita (6)** tangu kufunguliwa kwake. Hadi tunafunga mwaka 2018, Mahakama za Mwanzo zilipokea jumla ya mashauri

**176,652** na kumaliza mashauri **175,572** na kubakiza mashauri **15,675**. Mahakama za Mwanzo kwa mwaka 2018 zimesajili asilimia **71.3** ya mashauri yote yaliyosajiliwa mahakamani ambayo ni mashauri **247,596**. Hii inaonesha kuwa mahakama za mwanzo ndio hutumiwa zaidi na wanachi wengi wa kawaida mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Rais**, kati ya mashauri **15,675** yaliyobaki kwenye Mahakama za Mwanzo, ni mashauri **16** tu ndio yana umri zaidi ya miezi **6** (ili yaitwe mlundikano) ambao ni sawa na asilimia **0** ya mashauri yenye muda mrefu mahakamani (Mlundikano).

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama za Wilaya na za Hakim Mkazi nazo kwa kiwango kikubwa zilitekeleza lengo la kumaliza mashauri kwa haraka. Katika ngazi hii ya Mahakama lengo lilikuwa kuhakikisha mashauri yanasikilizwa na kumalizika ndani ya mwaka mmoja. Hadi mwisho wa mwaka 2018, Mahakama za Wilaya na za Hakim Mkazi zilikuwa zimepokea mashauri **51,161** na kumaliza Mashauri **47,089**, mashauri yaliyobaki ni **28,912**. Mashauri yaliyobaki, ni mashauri **837** (ambayo ni asilimia **5** ya Mashauri yenye muda mrefu mahakamani) yana zaidi ya mwaka mmoja mahakamani. Kati ya mashauri hayo yaliyo mengi ni yale ambayo Mahakama hizo hazina uwezo wa kuyasikiliza yanasubiri upelelezi ukamilike au yanasubiri kupelekwa katika Mahakama Kuu yenye mamlaka ya kuyasikiliza.



**Mheshimiwa Rais**, Mahakama Kuu iliwekewa sera ya kutakiwa kusikiliza mashauri na kuyatolea maamuzi ndani ya miaka miwili toka kufunguliwa kwake. Mahakama pia imejiwekea sera ya kumtaka kila Jaji kusikiliza angalau wastani wa mashauri **220** kwa mwaka. Mashauri yaliyobakia mwaka 2017 yalikuwa **19,187** na yaliyofunguliwa kwa mwaka 2018 yalikuwa mashauri **18,284** na hivyo kufanya jumla ya mashauri **37,471** yaliyotakiwa kusikilizwa na kumalizika mwaka 2018. Hata hivyo, ni mashauri **17,046** tu ndio yaliyomalizika na **20,425** yalibaki.

**Mheshimiwa Rais**, kwa kuzingatia idadi ya majaji **66** waliokuwepo hadi Desemba 2018, mzigo kwa kila Jaji ulikuwa wastani wa mashauri kwa kila Jaji ilikuwa **568**, idadi ambayo ni kubwa sana ikilinganishwa wastani wa mashauri **220** iliyopaswa kusikilizwa na kila Jaji. Baada ya Majaji wawili kustaafu, sita kupandishwa kwenda mahakama ya Rufani na kisha 15 kuapishwa na kuwa Majaji wa Mahakama kuu hivyo Jumla kuwa Majaji **73** katika Mahakama Kuu. Kwa kufuata idadi ya mashauri mwaka uliopita basi mzigo kwa kila Jaji wa Mahakama Kuu utashuka kidogo kutoka **568** hadi mashauri **513** kwa kila Jaji.

**Mheshimiwa Rais**, kwa mwaka 2018 Mahakama ya Rufani ilianza mwaka ikiwa na mashauri **2,933** yaliyobakia mwaka 2017 na ikafungua mashauri **1,499** na kusikiliza mashauri **1,184** na kubakia mashauri **3,248**. Takwimu zinaonesha kwamba kuna

ongezeko kubwa (ongezeko la mashauri **315**) kati ya mashauri yaliyosalia mwaka 2017 na yaliyosalia mwaka 2018. Tunakushukuru sana kwa kuongeza idadi ya Majaji wa Rufani, kutoka **15** waliokuwepo, hadi kufikia **20**.

**Mheshimiwa Rais**, pamoja na nyongeza ya Majaji, ni dhahiri kwamba hakuna uwiano kati ya mzigo wa kazi uliopo na idadi ya majaji wa Mahakama ya Rufani.

**Mheshimiwa Rais**, japo kujilinganisha na jirani yako laweza lisiwe sawa, hata hivyo, kwa kufuata matakwa na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, si vibaya kuangalia hali za majirani zetu. Kwa mfano, nchi ya Kenya yenye idadi watu wanaokadiriwa kufikia **milioni 50**, kuna jumla ya Majaji wa Mahakama Kuu **129**, Majaji **19** wa Mahakama ya Rufani na **7** wa Mahakama ya Juu (**Supreme Court**). Nchi ya Uganda, yenye idadi ya watu wanaokadiriwa kufikia **milioni 43**, wao kuna Majaji **59** wa Mahakama Kuu, **15** wa Mahakama ya Rufani na **11** wa Mahakama ya Juu (**Supreme Court**). Mwenyezi Mungu ametubariki kuwa na nchi kubwa. Kihasabu, ukubwa wa eneo la Nchi yetu ni sawa na ukubwa wa Kenya+Uganda+Rwanda+Burundi na kisha kujumlisha nusu nyingine ya Rwanda. Kwa hiyo, tunaweza kuona uwiano wa ukubwa wa eneo la nchi yetu na Majaji waliopo kuwa ni mkubwa sana. Hii ndio tafsiri ya Mashauri mengi yanayobaki kila mwaka.

## **Mashauri ya Kipaumbele**

**Mheshimiwa Rais**, kufuatia Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu kuwa na mlundikano wa mashauri, Mahakama hizi zililazimika kuyapatia kipaumbele mashauri mbalimbali. Mahakama ya Rufani iliyapatia kipaumbele mashauri ya mirathi ili kuhakikisha migogoro ya mirathi inatatuliwa haraka kutoa nafasi kwa warithi kunufaika mali za marehemu wazazi au mme au mke. Ningependa kuchukua fursa hii, kuishukuru Serikali yako kuwasilisha mabadiliko ya Sheria ambayo yameiruhusu Mahakama kuwapa Mamlaka ya ziada Mahakimu Waandamizi ili wasikilize mashauri ya Ardhi Mahakama Kuu.

**Mheshimiwa Rais**, mashauri mengine yaliyopewa kipaumbele ni mashauri ya kibiashara na kodi. Haya ni mashauri ambayo yakichelewa, huathiri urahisi wa kufanya biashara na kuathiri ukuaji wa uchumi na ustawi wa Wananchi. Mahakama ya Rufani kwa mwaka 2018 ilisikiliza mashauri kodi yenye thamani ya kodi inayobishaniwa ya kiasi cha shilingi **32,233,101,253/=** na dola za kimarekani **4,705,611**. Mashauri yaliyobaki mahakamani yamepangwa kusikilizwa mwezi Machi, 2019 pamoja na mashauri ya kibiashara. Kipaumbele pia imeelekezwa kwa mashauri ya jinai. Kwa mashauri ya jinai tunahakikisha mashauri hayo hayakai mahakamani zaidi ya miaka miwili.

## **Gharama ya ucheleweshwaji wa mashauri kwa Uchumi:**

**Mheshimiwa Rais,** pamoja na tafsiri nyingine, kauli mbiu inayotutaka tutoe haki kwa wakati, ina maana kwamba hapana ubishi kuwa ucheleweshwaji wa mashauri ya madai au ya jinai, yana gharama kubwa kwa uchumi wa nchi yoyote. Mahakama ndio sehemu ya mwisho ambayo wafanya biashara na wawekezaji wenye migogoro kuhusu mikataba ya biashara, kuhusu ardhi au migogoro ya uwekezaji; hukimbilia kutatua migogoro hiyo. Aidha, mara nyingi wakati mashauri yanapokuwa katika mlolongo wa kimahakama, matumizi ya mali husika na mgogoro, au fedha, au hata ardhi inayohusika na mgogoro; husimama kuisubiri ngazi husika ya Mahakama kukamilisha usikilizaji wa mgogoro, na mara nyingi migogoro hupitia ngazi zote za Mahakama husubiri hadi kusubiri uamuzi wa Mahakama ya Rufaa.

Kwa wafanya biashara, Mahakama yenye ucheleweshaji wa mashauri hujenga tabia mbaya kwa wafanya biashara wasio waaminifu kutoheshimu masharti ya mikataba ya biashara. Hutoa nafasi kwa wafanya biashara wasio waaminifu wavunje masharti ya mikopo. Ucheleweshaji wa kesi huyafanya Mabenki na Taasisi za Fedha kuwanyima wafanya biashara wadogo na wale wa ngazi ya kati, nafasi ya kupata mikopo. Mashauri kuchelewa imetajwa kama sababu mojawapo ambazo zinalazimisha Mabenki na Taasisi za Fedha kuweka masharti magumu ya mikopo, pamoja na kuweka masharti magumu ya riba katika mikopo inayotolewa. Kwa ufupi,

ucheleweshwaji wa mashauri hushamirisha ukiukwaji mkubwa wa sheria za kibiashara na huduma za uchumi.

**Mheshimiwa Rais,** wakati mwingine ucheleweshaji wa kesi Mahakamani kuhusu kesi za kibiashara, unatokana na milolongo mirefu ya kisheria na kimahakama. Nitatoa mfano wa mashauri ya kodi, yaliyofika Mahakama ya Rufani. Zipo ngazi TATU za Mahakama za KODI. Tathimini yetu ya mashauri ya kodi yaliyokuwa katika ngazi hizo tatu za Mahakama za Kodi kati ya tarehe **1 Januari 2017** hadi tarehe **30 Juni 2018** inaonyesha ni kwa kiasi gani Sheria zenye kuruhusu milolongo mirefu kabla ya shauri kukamilika, zinaweza kuwa kikwazo kwa kali mbiu yetu ya utoaji haki kwa wakati. Tathmini inaonyesha, Rufani Namba 95 ya 2017 ilidumu kwa jumla ya miezi **76** katika ngazi ya kwanza kabisa ya BODI YA RUFAA YA KODI (**Tax Revenue Appeals Board**). Rufaa Namba 99 ya 2017 ilikwama katika BODI YA RUFAA kwa miezi **72**; Rufaa Namba 100 ya 2017 ilikwama kwa miezi **48**; na Rufaa Namba 101 ya 2017 ilikwama kwa miezi **46**. Tathmini ya mashauri **14** ya kodi inaonyesha kuwa yalidumu kati ngazi ya Bodi kwa wastani wa **miezi 17**. Katika ngazi ya pili katika mfumo wa Mahakama za Kodi (Baraza la Rufaa za Kodi -**Tax Revenue Appeals Tribunal**) mashauri ya kodi yalidumu kwa wastani wa **miezi 23**. Tathmini inaonyesha kuwa katika ngazi ya mwisho ya Mahakama ya Rufani, mashauri ya kodi yalidumu kwa wastani wa **miezi 7**.

**Mheshimiwa Rais**, kwa kutumia kauli mbiu ya Mwaka huu (2019) **“Utoaji haki kwa wakati, Wajibu wa Mahakama na Wadau”**, wadau wa Mahakama wanaohusika na utungaji wa Sera za Kodi wanaweza kufanikisha utoaji haki kwa haraka zaidi ya ilivyo sasa kwenye mashauri ya Kodi, kwa kutathmini muda unaotumika katika NGAZI TATU za Mahakama za Kodi.

Licha ya mashauri ya kodi, Zipo sheria kadhaa kwenye mtiririko wa utoaji haki ambazo zinatakiwa kuangaliwa na wadau husika ili kupunguza mililongo na hatua nyingi kwa manufaa ya kupatikana kwa haki kwa wakati. Mfano mzuri hapa ni mashauri ya ardhi, ambayo yana ngazi NNE, kuanzia Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, Mahakama Kuu, hadi Mahakama ya Rufani.

#### **Mkakati wa kuondoa mlundikano wa mashauri:**

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama ya Tanzania ilidhamiria katika Mpango Mkakati wake kuondoa mlundikano wa mashauri mahakamani. Kwa kipindi cha miaka miwili sasa Mahakama imekuwa ikitekeleza mpango huo. Ninafurahi kukuarifu kuwa mpango huo umezaa matunda.

**Mheshimiwa Rais**, kabla ya kuanza kwa zoezi hili Mahakama ya Rufani ilikuwa na mashauri **999** ikiwa ni asilimia **37%** ya mashauri yote **2,700** mwishoni mwa mwaka 2016 yaliyokuwa ndani ya tafsiri ya mlundikano (yaani mashauri yaliyokaa Mahakamani zaidi ya

miaka miwili). Aidha, mashauri yalichukua wastani wa siku **5,240** kumalizika. Baada ya kuanza utekelezaji wa mpango huo, wastani wa siku za mashauri kusubiri kusikilizwa ulipungua hadi siku **1,241** mwishoni mwaka 2017.

**Mheshimiwa Rais**, baada ya kukamilisha zoezi la kuondoa mashauri kwa mwaka wa 2018 muda wa mashauri kusubiri kusikilizwa umepunguzwa hadi siku **1,098** (yaani wastani wa miaka mitatu kutoka wastani wa miaka **14** kabla ya zoezi kuanza). Hivyo basi, idadi ya mashauri ya mlundikano imepungua kutoka **999** mwaka 2016 hadi **729** kwa mwaka 2018.

**Mheshimiwa Rais**, haya ni mafanikio makubwa ingawaje yanaweza kuwa ya muda mfupi kwani kwa takwimu yapo mashauri mengi yenye miaka mitatu (3) yaani yaliyofunguliwa mwaka 2016. Aidha, mashauri yaliyobakia mwishoni mwa mwaka 2018 yameongezeka, kwa sasa ni **3,125** ukilinganisha na yaliyobaki mwaka 2016 ambayo yalikuwa **2,700**.

#### **Usimamizi na Ukaguzi wa utendaji wa kazi:**

**Mheshimiwa Rais**, kazi yoyote bora inategemea usimamizi bora, kwetu sisi inatendeka katika ngazi mbalimbali za mahakama kukfanya kazi za utoaji haki bila usimamizi, madhara yake ni makubwakwa **mustakabali** wa amani ya nchi na maendeleo ya

watu wake. Aidha, ili kupunguza **watumishi kujiamulia mambo kinyume na utaratibu** na vitendo vingine vya uvunjivu wa maadili kwa watumishi, Mahakama imedhamiria kuboresha usimamizi. Mahakama imetoa mafunzo juu ya njia bora ya kuendesha ukaguzi huo, imesambaza KITABU CHA MWONGOZO WA UKAGUZI.

**Mheshimiwa Rais**, kwa mwaka 2018 Mahakama za Hakimu Mkazi, Wilaya na Mwanzo zilikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo ni kuwa mashauri ya nidhamu yamependekezewa yafunguliwe dhidi maafisa wane kwakuwa walibainika kuvunja taratibu na maadili ili hatua sitahiki zichukuliwe.

Aidha, Mahakama iliendelea kusambaza vitabu vya mwongozo wa ukaguzi, mabango ya kuelimisha wananchi jinsi ya kuwasilisha malalamiko katika mahakama. Mpango wa kutolewa kwa elimu asubuhi angalau mara moja kwa wiki umeanzishwa katika Mahakama zote kwa wananchi wanaofika mahakamani katika mashauri yao. Aidha Mpango wa kusambaza nyaraka za kimahakama kupitia Mkataba wa Posta Mlangoni, umeanzishwa Machi 2018 na unatekelezwa ili wananchi wote wanaokuwa na kesi mahakamani na zikaisha wapate nakala zao za hukumu kwa wakati kwa kupelekewa mlangoni kwao.



**Mheshimiwa Rais,** kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa nakala za hukumu kwa wadaawa, hivyo Jaji Mkuu alitoa Waraka Maalum wa wadaawa kupewa nakala za hukumu bila malipo ndani ya siku **21** toka tarehe ambayo hukumu imesomwa. Waraka huo umerahisisha upatikanaji wa nakala hizo na kuweza kufaidi matunda ya tuzo wanazostahili au kukata rufaa kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais,** hata hivyo, mahakama iliendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa hukumu kwa Mhe. Jaji Mkuu kutoa maelekezo mengine kwa wasajili na wahe. Majaji wote wa Mahakama Kuu kuwa ***kila ifikapo tarehe 5 ya kila mwezi kila Jaji wa Mahakama Kuu awasilishe idadi ya maamuzi aliyoyatoa akiambatanisha na nakala husika kupitia kwa Msajili Mkuu na Kurugenzi ya Usimamizi wa Mashauri.*** Aidha, utaratibu huo unaendana sambamba na upimwaji wa utendaji kazi kwa wasajili na majaji husika kila ifikapo mwisho wa mwaka wa mahakama.

**Mheshimiwa Rais,** utaratibu huu hautaishia katika ngazi ya Mahakama Kuu tu bali unaendelea katika Mahakama za Mahakimu. Kwa ufupi, Mahakama imejiwekea sera kadhaa zinazosaidia upimaji wa utendaji wa watumishi wote kila wakati.

**Mheshimiwa Rais,** kwa muda mrefu, mahakama imekuwa ikihamasisha wananchi kupenda kufanya usuluhishi wa matatizo mbalimbali nje ya mahakama isipokuwa tu inapobidi kulifikisha suala lao mahakamani. Sambamba na hilo mahakama katika nyakati tofauti imetoa mafunzo kwa Majaji na Mahakimu ili kuhakikisha wanahamasisha usuluhishi kwa wadaawa ambao wamekwishafikisha kesi zao mahakamani kwa zile kesi ambazo sheria inaruhusu usuluhishi. Huduma ya Usuluhishi una faida kadhaa ambao husaidia kujenga kauli mbiu ya upatikanaji wa haki kwa wakati:

- (a) Shauri linaisha siku hiyo ya usuluhishi na wahusika wanabaki na ujirani mwema, undugu na urafiki usio na uadui.
- (b) Huepusha gharama zitokanazo na kusikilizwa na shauri kuanzia ngazi za chini za Mahakama hadi Mahakama ya Rufani.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa kuzingatia kwamba suala la usuluhishi mahakamani ni takwa la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 107A, inayosomeka

*“katika kutoa maamuzi ya mashauri ya madaai,  
kwa kuzingatia sheria, mahakama zitafuata  
kanuni zifuatazo: yaani kukuza na kuendeleza*

*usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro”,*

Hivyo basi mnamo mwaka 2015 Mahakama ya Tanzania ilianzisha Kitengo cha Usuluhishi (*Mediation Centre*) ndani ya Mahakama Kuu kwa lengo la kukua majadiliano ya kumaliza migogoro nje ya mahakama katika jamii na lakini pia kusaidia kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani na kukamilisha kesi kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais**, hadi kufikia mwezi November 2018, Kitengo cha Usuluhishi kilikuwa kimepokea mashauri **715** ambapo mashauri **649** sawa na asilimia **91** ndiyo yalishughulikiwa.

**Mheshimiwa Rais**, Divisheni ya Makosa ya Rushwa ya Uhujumu Uchumi ilianzishwa Julai 2016, kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura Namba 200 iliyofanyiwa mabadiliko na Sheria ya Mabadiliko ya Sheria mbalimbali Namba **3/2016**. Divisheni ilianza kusajili mashauri tarehe 27/10/2016 katika Masjala ya Divisheni hiyo iliyopo Dar es Salaam na baadae mashauri yalianza kusajiliwa katika Masjala ya Dar es Salaam na Masjala ndogo zilizoko katika Kanda mbalimbali za Mahakama Kuu.

**Mheshimiwa Rais,** Mashauri mengi ambayo yamesajiliwa katika Divisheni yanahusu maombi ya Dhamana hali inayoonesha kwamba kwa siku za usoni Divisheni itakuwa na idadi kubwa ya mashauri endapo upelelezi utakamilika katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya ambako mashauri hayo huanzia katika hatua za awali.

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi pia imesajili mashauri asilia ya uhujumu uchumi katika Masjala zake mbalimbali na takwimu za miaka mitatu mfululizo toka ianzishwe zinaonesha kama ifuatavyo; maombi ya dhamana mwaka 2016 yalisajiliwa nane **(8)**, yalimalizika nane **(8)**; mwaka 2017 maombi ya dhamana yalisajiliwa **148** na yalimalizika maombi 147 na ombi moja **(1)** lilibaki; mwaka 2018 yalisajiliwa maombi ya dhamana **223**, yalimalizika **201** na kubaki maombi **22**.

**Mheshimiwa Rais,** mashauri ya uhujumu uchumi kwa mwaka 2017 yalisajiliwa mashauri saba **(7)** na kumalizika matano **(5)** na mawili **(2)** yanaendelea; mwaka 2018 yalisajiliwa mashauri thelathini na tano **(35)** yakamalizika mashauri sita **(6)** na mashauri ishirini na tisa **(29)** bado yanaendelea kusikilizwa.

**Mheshimiwa Rais,** Mahakama zinazotembea ni dhana inayomaanisha mahakama katika ngazi fulani kuhamisha huduma zake na kuzitolea katika sehemu mbalimbali ndani ya mamlaka yake. Mfano rahisi ni pale Mahakama ya Rufani inapohamisha shughuli zake kutoka Dar es Salaam kwenda katika vituo mbalimbali ndani ya mamlaka yake au Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma inapohamishia shughuli zake Wilaya ya Kongwa, Kondoa au Singida.

**Mheshimiwa Rais,** dhana hii imekuwepo toka siku za nyuma ambapo Mahakama Kuu ilitumia behewa la treni kutoa huduma za kimahakama kwenye ukanda ambao treni ilipita. Mahakama hiyo ilianzishwa mwaka 1920 na sababu za kuhamisha mahakama zilikuwa kumfuata shahidi kwa sababu ni mgonjwa au kuwapunguzia gharama mashahidi au iwapo kielelezo hakihamishiki kirahisi.

**Mheshimiwa Rais,** kwa sasa Mahakama zinazotembea zinamaanisha kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi hasa sehemu zisizo na mahakama kusikiliza kesi na kuzimaliza. Katika dhana hii mpya (**ya Mobile Courts**) mahakama itahamishia shughuli zake katika chumba maalumu kilichotengenezwa ndani ya gari lakini kuna huduma zote muhimu kama ilivyo ofisi au “*chambers*” ya hakimumu ambapo itasikiliza mashauri na kuyatolea maamuzi.

**Mheshimiwa Rais**, mahakama hii ni gari maalumu lenye sehemu mbili (2) **Chumba cha hakim** kitakuwa na meza ya hakim, meza ya wadaawa, meza ya karani/mpiga chapa, Televisheni, Kompyuta “Printer”, Kabati la kutunzia majalada, Vyombo vya kurekodi mashauri na vifaa vya kutangazia (vipaza sauti) pamoja na chumba cha faragha.

**Mheshimiwa Rais**, katika awamu ya kwanza (*Pilot Study*) yamenunuliwa magari mawili (2) yatakayotoa huduma katika mikoa ya Dar es salaam na Mwanza. Katika Mkoa wa Dar es salaam, Wilaya ya Kinondoni kituo kitakuwa **Bunju**, Wilaya ya Ilala –**Chanika**, Wilaya ya Temeke - **Buza** na **Kibamba** katika Wilaya ya Ubungo. Katika mkoa wa Mwanza Wilaya ya Ilemela kituo kitakuwa **Buhongwa** na **Igoma**, kwa Wilaya ya Nyamagana kituo kitakuwa **Buswelu**. Magari hayo, Mhe. Rais yapo hapa na umeyazindua leo hii tayari kwenda vituoni kuanza kazi.

**Mheshimiwa Rais**, dhamira yetu ya baadae ni kuwa na magari ya aina hii nchi nzima kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi kwa mfano jamii za wafugaji na wavuvi ili kuwapunguzia wananchi wote kero. Mahakama hizi zitakuwa chini ya mamlaka ya Mahakama husika za Wilaya na Mwanzo na Mahakimu walioteuliwa kuzisimamia wamepatiwa mafunzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna ya kuhudumia wateja (**customer care**).

Mahakama inayotembea inatarajiwa kuwa kimbilio la wananchi wengi kwa huduma nzuri zitakazotolewa katika mahakama hizi.

## **6.0 Utoaji Haki kwenye Mabaraza na Tume**

**Mheshimiwa Rasi,** kama nilivyosema awali, utoaji haki ni suala mtambuka na linagusa taasisi nyingi. Hata hivyo, taasisi hizo zisipofanya kazi vizuri, lawama inarudi Mahakamani. Kwa mfano, utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ni changamoto kubwa. Pamoja na uwepo wa idadi ndogo ya watenda kazi kwenye Mabaraza hayo, bado sheria yake ina changamoto kwenye usimamizi, nidhamu na uwajibikaji wao. Wananchi hawajui tofauti ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba na Mahakama. Mara nyingi tunapokea malalamiko ya Mabaraza ya Arhdi lakini kwa mujibu wa sheria, hawawajibiki kwangu. Tunaona kuna kila sababu kufanyia kazi mapendekezo mbali mbali juu wa Mabaraza ya Ardhi.

## **7.0 Miundombinu ya majengo**

**Mheshimiwa Rais,** mahakama inaendelea kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi kwa kujenga majengo mapya na matarajio ni kwamba ifikapo mwezi Juni 2019 jumla ya majengo **52** ya Mahakama yatakuwa yamekamilika kwenye maeneo mbalimbali nchini yakiwemo ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu.

Majengo yanayoendelea kujengwa ni pamoja na Mahakama za Mwanzo **22**, Mahakama za Wilaya **20**, Mahakama za Mikoa (Hakimu Mkazi) **8** pamoja na Mahakama Kuu **2**, zinazojengwa katika mikoa ya Mara na Kigoma.

**Mheshimiwa Rais**, Baadhi ya majengo yamekamilika na mengine yako katika hatua za mwisho za ukamilishwaji huku mengine yakiwa katika hatua za awali kabisa za ujenzi. Majengo yaliyokamilika ni yale yaliyokuwa kwenye mpango wa ujenzi katika mwaka wa fedha wa 2016/2017. Majengo yaliyokamilika na kuzinduliwa mwaka 2018 ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Pwani na Mahakama ya Wilaya ya Kibaha, Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni; na Mahakama ya Mwanzo Kawe. Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Ilala lililopo eneo la litazinduliwana Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mbunge), Waziri wa Katiba na Sheria, katika tarehe itakayopangwa hivi karibuni.

**Mheshimiwa Rais**, katika mwaka wa fedha 2017/2018 mahakama ilikamilisha mradi wa ujenzi wa majengo **12** ambayo ujenzi wake ulisimama katika miaka ya nyuma. Miradi hiyo ni ile inayojumuisha Mahakama za Hakimu Mkazi (Mkoa wa Manyara), Mahakama za Wilaya pamoja na Mahakama za Mwanzo **Iguguno (Singida)**, **Wasso (Loliondo)**, **Old Korogwe** na **Magoma (Korogwe)**, **Karatu**, **Robanda (Serengeti)**, **Itinje (Meatu)** na **Totoe (Songwe)**.



Aidha, Mahakama ya Tanzania pia ilikamilisha miradi ya ukarabati mkubwa wa majengo yake ya Mahakama Kuu ya Tanzania yaliyopo **Mbeya**, Mahakama ya Biashara (**Mwanza**) na Makazi ya Jaji Mfawidhi (**Dodoma**).

**Mheshimiwa Rais**, vilevile katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 tulianza kujenga majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi katika mikoa yote mipya yaani **Geita, Njombe, Simiyu, Katavi** pamoja na Mkoa wa **Lindi**. Ujenzi katika mikoa hiyo unaendelea. Sambamba na hilo, ujenzi wa miradi **16** ya Mahakama za wilaya nchini unaendelea zikiwemo wilaya za **Geita, Njombe, Bariadi, Lindi, Mpanda, Rungwe** na **Ruangwa**. Mahakama nyingine za wilaya zinazojengwa ni **Chato, Bukombe, Bunda, Kasulu, Sikonge, Kilwa Masoko, Kondo, Longido** na **Kilindi**.

**Mheshimiwa Rais**, tumeanza kutekeleza azma yetu ya kuwa na Mahakama Kuu katika kila Mkoa na tayari tumeanza ujenzi wa Majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya **Mara** (Musoma) na **Kigoma**. Ujenzi huo umefikia hatua za mwisho na majengo hayo yanatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili; 2019.

**Mheshimiwa Rais**, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inakusudia kuendelea kusogeza huduma za Mahakama karibu

zaidi na wananchi kwa kujenga majengo sita **(6)** ya Mahakama Kuu maarufu kama “vituo vya utoaji wa Haki Jumuishi”(**Intergrated Justice Centre**) katika mikoa ya **Morogoro, Dodoma, Mwanza na Arusha**. Aidha, katika jiji la Dar es Salaam, Mahakama itajenga Majengo hayo katika wilaya ya **Temekena** kwenye viwanja vya Mahakama vya **Chimala** vilivyopo jirani na Hospitali ya Ocean Road.

**Mheshimiwa Rais**, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Mahakama ya Tanzania imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya **Mtae (Lushoto), Mdandu (Wanging’ombe), na Mkunya (Newala), Msanzi, Laela na Mtowisa (Sumbawanga), Uyole (Mbeya), Mlimba, Mang’ula na Ngerengere (Morogoro)**.

Vilevile Mahakama imepanga kujenga Mahakama za Wilaya katika Wilaya za **Chunya (Mbeya), LudewanaMakete (Njombe)**.

## **8.0 Bajeti ya Mwaka 2018/19 na Mahitaji ya 2019/20**

**Mheshimiwa Rais**, bajeti ya Mahakama kwa mwaka 2018/19 ni shilingi **141,584,737,540** kati ya hizo, shilingi**52,754,477,540** ni mishahara ya watumishi, shilingi **1,875,156,000** kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, na shilingi **50,981,382,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi

cha shilingi **15,000,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (fedha za ndani) na shilingi **20,973,722,000** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (fedha za nje).

**Mheshimiwa Rais**, bajeti ya Matumizi Mengineyo (OC) iliongezeka kwa asilimia 0.99 ikilinganishwa na ile ya 2017/18, ongezeko ambalo ni kidogo sana ikilinganishwa na ongezeko la gharama za uendeshaji, na mahitaji ya msingi yaliyowasilishwa na Mahakama.

**Mheshimiwa Rais**, eneo linalohitaji maboresho katika uendeshaji wa Mahakama ni ongezeko la majaji ambalo litakwenda sambamba na ongezeko la fedha. Mahitaji yatakayoambatana na kuapishwa kwa Majaji wapya ni pamoja na ununuzi wa magari, nyumba, samani, laptops, mafunzo (*orientation*), na uhamisho kuelekea vituoni, ambapo gharama za nyongeza zitakazohitajika ni **Tshs. 11,095,000,000.00**. Kiasi hiki kimeombwa kwenye mapitio ya nusu mwaka (mid-year review) kwa kuwa haya matumizi yanatarajiwa kabla ya Juni 2019.

**Mheshimiwa Rais**, kama nilivyoeleza hapo awali, baadhi ya maeneo yaliyokosa fedha mwaka 2018/19 yaliahirishwa kutekelezwa, lakini hata hivyo umuhimu wake ni mkubwa. Ili kukidhi mahitaji yake, Mahakama inaomba kuongezewa ukomo wa bajeti kwa mwaka **2019/20** katika maeneo yafuatayo:-

ProgramuMaalum ya Kupunguza Mlundikano wa Mashauri **sh. 3,843,790,800**; Posho za Wazee wa Baraza (Mahakama za Mwanzo) **sh. 750,000,000**; uanzishwaji wa Mahakama katika Wilaya **28** zisizokuwa na Mahakama **sh. 4,555,800,000**; posho ya pango kwa Mahakimu wote **sh. 5,040,000,000**; Posho ya Majukumu kwa Mahakimu wafawidhi wa Mkoa na Wilaya **sh. 644,000,000**; uhamisho wa watumishi waliokaa kituo kimoja muda mrefu **sh. 3,040,000,000**; na maombi ya nyongeza ya Fedha za ndani za Maendeleo sh. **9,000,000,000**.

**Mheshimiwa Rais**, naomba nigusie kidogo kuongezewa ukomo wa bajeti kwa mwaka **2019/20** ili Wilaya za kiutawala **28** zipate Mahakama za Wilaya. Nilikumbushwa umuhimu wa kila Wilaya iwe na Mahakama ya Wilaya pale nilipotembelea Wilaya ya Uvinza mwaka jana (2018). Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Bi.Mwanamvua Mlindoko, alielezea athari za kukosekana kwa Mahakama ya Wilaya katika wilaya ya Uvinza: **MOJA**, ugumu wa kushughulikia makosa makubwa ya kijinai hasa katika maeneo ya mipakani mwa nchi, makosa haya ni pamoja na uhujumu uchumi; mauaji; unyang'anyi wa kutumia silaha; na uhamiaji haramu. Haya makosa ni lazima yafikishwe kwanza Mahakama za Wilaya (kwa hatua za awali) kabla ya kupelekwa kusikilizwa Mahakama Kuu au Mahakama Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; **MBILI**, msongamano wa mahabusu katika kituo cha polisi Uvinza ili kusubiri kusafirishwa kwenda Mjini Kigoma ambayo kuna Mahakama ya Wilaya; **TATU**, gharama inaongezeka kwa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na

Uhamiaji kuwasafirisha watuhumiwa kwenda Kigoma; na **NNE**, kesi kubwa kubwa kufutwa kutokana na mashahidi kushindwa kusafiri hadi Kigoma kuhudhuria vikao vya Mahakama ya Wilaya.

**Mheshimiwa Rais**, ombi la kuongezewa ukomo wa bajeti kwa mwaka **2019/20** kwa ajili ya posho ya **Wazee wa Baraza** katika Mahakama za Mwanzo ina umuhimu sana katika wajibu wa Mahakama katika Utoaji haki kwa wakati katika Mahakama za Mwanzo, na pia wajibu wa Serikali kama Mdau anayeiwezesha Mahakama itoe haki kwa wakati.

Kwa mujibu wa Sheria, kila kesi zinazosikilizwa Mahakama za Mwanzo, ni lazima ziwahusishe Wazee wa Baraza wawili, ambao hulipwa shilingi elfu tano (**5,000/=**) **kila mmoja**, sio kila siku, bali pale kesi wanayosikiliza ikimalizika. Kiwango hiki ni kidogo sana ikilinganishwa na muda wazee hawa wanaotumia kuja mahakamani kila siku hadi kesi husika inapokamilika. Pamoja na udogo wa kiwango cha shilingi elfu tano, wakati mwingine Mahakama zimeshindwa kuzilipa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Kwa mfano, katika mwaka **2017/18**, Mahakama ilifunga mwaka ikiwa na deni la Wazee wa Baraza la takriban shilingi **115 milioni**. Changamoto hii ya madeni kwa Wazee wa Baraza itazidi kuongezeka kwa sababu katika mwaka 2017/18, ujenzi wa idadi ya Mahakama za Mwanzo zipatazo **tisa (9)** zilikamilika katika sehemu mbali mbali ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Rais**, nitakua mchoyo wa fadhila nisipo washukuru wadau wawili muhimu, Mhe. Job Ndugai Spika (Mb), Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria, ambao wamefanikisha kutungwa kwa Sheria kadhaa, pamoja na kanuni ambazo zimeboresha mazingira ya utoaji haki kwa wakati. Hapa, nitaje mfano wa **Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali Namba 8 ya 2018** [*Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Act, 2018*] ambayo yameingiza katika mfumo wa utoaji haki, msingi wa kisheria uitwao, “*Overriding Objective*”—(*Lengo Kuu la kuzingatiwa na wote wanaohusika katika mfumo wa utoaji haki*). Kwa ufupi, pamoja na kulenga kuhakikisha kuwa mashauri yanayofikishwa Mahakamani hayaishii katika kuondoshwa kwa kuzingatia sababu za kiufundi, msingi wa OVERRIDING OBJECTIVE inawalazimisha Majaji, Mahakimu, Wasajili, Mawakili, na Wadaawa wote, waelewe lengo kuu la Mahakama za Tanzania ni—**MOJA**, kuwezesha ufanisi katika utoaji haki, **PILI**, haki ipatikane kwa wakati, **TATU**, haki isipatikane kwa gharama kubwa na **NNE**, Mahakama na wadau katika kila shauri, wahakikishe kuwa mgogoro halisi ulioletwa katika ngazi husika ya mahakama yanakamilika na sio kuondoshwa kwa sababu za kiufundi.

## **9.0 Mwisho**

**Mheshimiwa Rais,** Nawashukuru Majaji wa Rufani, Majaji wa Mahakama Kuu, Mahakimu, Watendaji, Watumishi wote wa Mahakama, Mawakili wa Serikali, Mawakili wa Kujitegemea na wadau wengine wote—kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuleta maendeleo ya Nchi yetu kupitia utoaji wa haki.

Aidha, napenda nichukue fursa hii ya kipekee, na kwa heshima kubwa, kukushuru wewe binafsi kwa kuhakikisha kuwa Mhimili wa Mahakama unapata rasilimali ya kuiwezesha kutoa haki. Nakushukuru kwa kukubali wito wetu wa kuja kujiunga nasi SIKU HII YA SHERIA.

**Mheshimiwa Rais,** Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliuzindua tarehe 21 September, 2016 umefikia miaka mitatu ya utekelezaji, nina diriki kusema, kwa mafanikio makubwa. Somo muhimu ambalo limetokana na utekelezaji wa Mpango Mkakati ni kwamba, viongozi wa Mahakama na viongozi wa Taasisi-Wadau katika utoaji haki, kazi zetu sio kulalamika na kulaumu. Wajibu wetu mkubwa ni kusikiliza na kutambua changamoto katika utoaji haki, kuyafanyia kazi, kwa kujipa muda wa kutatua hizo changamoto. Katika hotuba aliyoitoa tarehe 19 Octoba 1960 akiwa kama Waziri Kiongozi wa Tanganyika, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alionyesha kuchukizwa sana na tabia iliyokuwa ikijengeka wakati huo, ya kupenda kulaumu wengine hasa ambao tumepewa mamlaka ya

kikatiba na kisheria ya kutatua changamoto tunazolalamikia. Alisema kulalamika lalamika ni mabaki ya akili za kikoloni- ***“There is nobody now we can blame. We have been trained now to blame and we come here and since we are used to blame and we are here to blame... This is a colonial mind. From now on you have to blame yourselves and no one else.”***

**Mheshimiwa Rais**, Kama Baba wa Taifa alivyotuasa, Mpango Mkakati wa Mahakama unatusaidia kuacha kulaumu wengine, bali tupange mikakati na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi, naomba, nikukaribishe sasa utuzindulie (waingereza wanaita STRATEGIC INTERVENTION)– MFUMO WA KIELEKTONIKI WA KURATIBU MASHAURI (**JSDS II**) na kisha utupatie nasaha zako kwenye siku hii muhimu kwa Mahakama na kwa Wanajumuiya wa Sekta ya Sheria na Wananchi kwa ujumla karibu sana Mheshimiwa Rais.

***“Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.”***

***“Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.”***